



kuku na jongoo Chicken and Millipede



✎ Winny Asara
🔊 Magriet Brink
📄 Matteo E. Mwita
🗣️ Kiswahili / English
📊 Level 3


This story originates from the African Storybook (africanstorybook.org) and is brought to you by Storybooks Canada in an effort to provide children's stories in Canada's many languages.



This work is licensed under a Creative Commons

[Attribution 3.0 International License.](https://creativecommons.org/licenses/by/3.0)

<https://creativecommons.org/licenses/by/3.0>



Kuku na Jongoo walikuwa marafiki. Ila walikuwa wanashindana kila mara. Siku moja wakaamua kucheza mpira wa miguu ili waweze kubaini nani alikuwa mchezaji bora zaidi.

...

Chicken and Millipede were friends. But they were always competing with each other. One day they decided to play football to see who the best player was.



Wakaenda uwanjani na wakaanza kucheza. Kuku alikuwa na kasi ila jongoo alikuwa na kasi zaidi. Kuku alipiga mpira mbali, ila jongoo alipiga mbali zaidi. Kuku akaanza kupandwa na hasira.

...


They went to the football field and started their game. Chicken was fast, but Millipede was faster. Chicken kicked far, but Millipede kicked further. Chicken started to feel grumpy.



Wakaamua kupigiana penati. Jongoo akaenda golini. Kuku alifunga goli moja pekee. Ikawa zamu ya kuku kwenda golini.

...

They decided to play a penalty shoot-out. First Millipede was goal keeper. Chicken scored only one goal. Then it was the chicken's turn to defend the goal.



Tangu hapo, Kuku na Jongoo ni maadui.

...

From that time, chickens and millipedes were enemies.



Jongoo alipiga mpira akafunga. Jongoo akapiga chenga akafunga. Jongoo akapiga kichwa akafunga. Jongoo akafunga magoli matano.

...

Millipede kicked the ball and scored. Millipede dribbled the ball and scored. Millipede headed the ball and scored. Millipede scored five goals.



Kuku alikohoa, hadi akamtema jongoo aliyekuwa tumboni mwake. Mama jongoo na mwanaye wakashwa mti kujificha.

...

Chicken coughed until she coughed out the millipede that was in her stomach. Mother Millipede and her child crawled up a tree to hide.



Kuku akakasirika kwa kuwa amefungwa. Hakuwa mshindani mzuri. Jongoo akaanza kucheka kwa sababu rafiki yake alikuwa analalamika.

...


Chicken was furious that she lost. She was a very bad loser. Millipede started laughing because his friend was making such a fuss.



Kuku akabeuwa. Akameza mate na kutema. Halafu akapiga chafya na kukohoa. Akakohoa tena. Jongoo alimfanya ajisikie vibaya.

...

Chicken burped. Then she swallowed and spat. Then she sneezed and coughed. And coughed. The millipede was disgusting!



Kuku alipatwa na hasira kiasi kwamba akafungua mdomo wake mkubwa na akammeza jongoo.

...

Chicken was so angry that she opened her beak wide and swallowed the millipede.



Mama Jongoo alipiga kelele, "Tumia nguvu yako ya kipekee mwanangu!" Majongoo wanaweza kutoa harufu mbaya na ladha ya ajabu. Kuku akaanza kujisikia mgonjwa.

...


Mother Millipede shouted, "Use your special power my child!" Millipedes can make a bad smell and a terrible taste. Chicken began to feel ill.



Kuku alipokuwa anarudi nyumbani alikutana na Mama yake Jongoo. Mama Jongoo akamuuliza, “Umemwona mwanangu?” Kuku hakujibu kitu. Mama Jongoo akapatwa na wasiwasi.

...

As Chicken was walking home, she met Mother Millipede. Mother Millipede asked, “Have you seen my child?” Chicken didn’t say anything. Mother Millipede was worried.



Mama Jongoo akasikia sauti kwa mbali. “Nisaidie mama!” ile sauti ililia. Mama Jongoo akaangalia huku na kule na kusikiliza kwa makini. Sauti ilitokea tumboni mwa kuku.

...

Then Mother Millipede heard a tiny voice. “Help me mom!” cried the voice. Mother Millipede looked around and listened carefully. The voice came from inside the chicken.